

HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE



Zabuni namba. LGA/016/2017-18/HQ/NC/06

YA

UNUNUZI WA HUDUMA YA ULINZI

Mwaliko wa zabuni.

Tarehe: **18 Mei, 2017**

1. Halmashauri ya Manispaa ya Temeke inalojukumu la kuhakikisha ulinzi na usalama wa majengo na samani za ofisi zilizomo kwa mwaka wa fedha 2017/2018, kutokana na uhaba wa fedha imeamua kubinafsisha jukumu hili kwa makampuni binafsi.
2. Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, inawaalika watoa huduma wote wa ndani ya nchi na wenye sifa na uwezo wa kutoa huduma ya ulinzi waje kuomba kazi hii.
3. Njia ya ununuzi itakayofanyika ni ya ushindani kwa watoa huduma wa ndani kitaifa (NCT) na taratibu zitakazotumika ni kwa mujibu wa kanuni namba 446 za mwaka 2013.
4. Watoa huduma wenye nia wanaweza kupata taarifa na kukagua makabrasha ya zabuni ofisi ya katibu wa bodi ya zabuni ya Manispaa ya Temeke, sanduku la posta 46343, barabara ya Mandela/Taifa, Dar Es Salaam kuanzia saa 3:00 asubuhi hadi saa 09:30 jioni kuanzia jumatatu hadi ijumaa kwa siku za kazi tu.

5. Kabrasha la zabuni kwa lugha ya kiswahili linaweza kununuliwa na watoa huduma wenye nia pamoja na barua ya maombi kwa kutumia anuani iliyooneshwa hapo juu aya ya nne kwa malipo ya 100,000/= yasiyorudishwa. Malipo yanaweza kufanywa kwa njia ya fedha taslimu mlipwaji ni Mkurugenzi Mtendaji wa Manispaa, Manispaa ya Temeke.
6. Zabuni zote lazima ziambatishwe pamoja na hati ya dhamana ya zabuni (tender securing declaration) ikiwa katika muundo ulioambatanishwa kwenye kitabu cha zabuni
7. Zabuni zote halisi pamoja na nakala mbili zilizofungwa vizuri kwenye bahasha ziwasilishwe kwa anuani ya Mkurugenzi Mtendaji, Manispaa ya Temeke, Sanduku la Posta 46343, barabara ya Mandela/Taifa, Dar Es Salaam kwenye ukumbi wa kitengo cha Ununuzi kabla ya saa 5.00 asubuhi siku ya Ijumaa tarehe 02/06/2017, Zabuni zitafunguliwa mara baada ya muda wa kupokelewa kuisha mbele ya wawakilishi wa watoa huduma waliochagua kuhudhuria ufunguzi kwenye ukumbi wa Kitengo cha Ununuzi katika Manispaa ya Temeke, sanduku la posta 46343, barabara ya Mandela/Taifa, Dar Es Salaam.
8. Zabuni zitakazochelewa, zabuni zitakazotumwa kwa mtandao hazitopokelewa, zabuni ambazo hazikufunguliwa wala kusomwa kwenye ufunguzi haitofanyiwa tathmini na pia zitarudishwa kwa wahusika.

Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Manispaa ya Temeke